**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Utekelezaji wa Mitalaa ya Kiswahili Vyuoni na Namna Unavyoathiri Utendakazi wa Walimu Wanaofundisha katika Shule za Upili.

*Jackline Mwanzi[1], Prof. Odeo Isaac Ipara, PhD[1] & Prof. Kenneth Inyani Simala, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-8319-1671; Barua pepe ya mawasiliano: jacklinemwanzi@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*18 Februari 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Mitalaa, Utekelezaji, Utendakazi, Walimu.*

## IKISIRI

Walimu wanaofundisha katika shule za upili hupata mafunzo yao ya kitaaluma kutoka katika vyuo vikuu mbalimbali. Wanapoandaliwa vyuoni, walimu hawa hupewa mafunzo kwa kutumia mitalaa tofauti inayoandaliwa katika vyuo vikuu hivyo. Baada ya kuhitimu, wao hutarajiwa kuutekeleza mtalaa mmoja unaoandaliwa na Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa nchini Kenya (TUMIKE) ili ufundishwe katika shule zote za upili. Utafiti ulifanywa ili kudhihirisha iwapo mafunzo ya kitaaluma yanayotolewa vyuoni kuwaandaa walimu wa somo la Kiswahili yanawapa maarifa na stadi wanazohitaji kufundisha katika shule za upili baada ya kuhitimu. Makala haya yametokana na utafiti uliofanywa ili *Kutathmini uhusiano baina ya mitalaa ya Kiswahili inayotumika katika vyuo vikuu vya umma nchini Kenya na mtalaa ambao umeandaliwa na TUMIKE ili kutekelezwa katika shule za upili.* Utafiti ulifanyika katika vyuo vikuu vitano vya umma nchini Kenya. Muundo wa utafiti ulikuwa usoroveya elezi. Data ilikusanywa kwa njia ya usaili, uchanganuzi wa nyaraka na hojaji. Uchanganuzi wa data ulikuwa wa kitakwimu na kimaelezo. Utafiti uligundua kuwa uhusiano baina ya mitalaa rasmi ya Kiswahili ya vyuo vikuu vya umma na mtalaa wa Kiswahili wa shule za upili siyo wa moja kwa moja. Hali hii iliathiri utendakazi wa walimu walipotekeleza mtalaa wa shule za upili. Uhusiano mdogo uliopo baina ya mitalaa rasmi ya vyuo vikuu na mtalaa rasmi wa TUMIKE ulidhihirika kwa kuchunguza vipengele vikuu vya mtalaa ambavyo ni: malengo, mada, utekelezaji na tathmini. Utafiti unapendekeza pafanyike marekebisho ya mara kwa mara ya mtalaa wa TUMIKE kwa kuwahusisha walimu na waandalizi wao ili wakadirie malengo, mada, mbinu za utekelezaji na tathmini mintarafu maandalizi yanayotolewa kwa walimu.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

**APA CITATION**

Mwanzi, J., Ipara, O. I., & Simala, K. I. (2022). Utekelezaji wa Mitalaa ya Kiswahili Vyuoni na Namna Unavyoathiri Utendakazi wa Walimu Wanaofundisha katika Shule za Upili. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 25-38. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556.

**CHICAGO CITATION**

Mwanzi, Jackline, Odeo Isaac Ipara & Kenneth Inyani Simala. 2022. "Utekelezaji wa Mitalaa ya Kiswahili Vyuoni na Namna Unavyoathiri Utendakazi wa Walimu Wanaofundisha katika Shule za Upili". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 25-38. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556.

**HARVARD CITATION**

Mwanzi, J., Ipara, O. I., & Simala K. I. (2022) "Utekelezaji wa Mitalaa ya Kiswahili Vyuoni na Namna Unavyoathiri Utendakazi wa Walimu Wanaofundisha katika Shule za Upili", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 25-38. doi: 10.37284/jammk.5.1.556.

**IEEE CITATION**

J. Mwanzi, O. I. Ipara, & K. I. Simala, "Utekelezaji wa Mitalaa ya Kiswahili Vyuoni na Namna Unavyoathiri Utendakazi wa Walimu Wanaofundisha katika Shule za Upili", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 25-38, Feb. 2022.

**MLA CITATION**

Mwanzi, Jackline, Odeo Isaac Ipara & Kenneth Inyani Simala. "Utekelezaji wa Mitalaa ya Kiswahili Vyuoni na Namna Unavyoathiri Utendakazi wa Walimu Wanaofundisha katika Shule za Upili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Feb. 2022, pp. 25-38, doi:10.37284/jammk.5.1.556.

## UTANGULIZI

Mchakato wa kuwaandaa walimu wa shule za upili unakumbwa na changamoto nyingi kote ulimwenguni. Goodlad (1995,1984) anasema kuwa maandishi mengi kuhusu taaluma ya elimu yameibua mijadala kuhusu changamoto zinazodhihirika katika maandalizi ya walimu wa shule za upili. Baadhi ya changamoto hizo huwaathiri walimu wanapotekeleza mitalaa ya shule za upili.

Utafiti uliofanywa na Miller na Silvernail (2000) unaonyesha kwamba namna walimu wa shule za upili walivyofunza baada ya kuhitimu hakuambatani na mafunzo ya ualimu waliyoyapokea katika vyuo vikuu. Miller na Silvernail wanasema kwamba yale ambayo walimu huyafanya wanapokuwa nyanjani kutekeleza yaliyomo kwenye mitalaa ya shule za upili ni mambo ambayo wanajua yanatarajiwa kutoka kwao kama walimu na wala hawayahusishi na mafunzo ya ualimu waliyoyapata.

Lynch (2003) anasema kwamba utafiti uliowahi kufanyika katika chuo kikuu kimoja kulinganisha njia za ufundishaji zilizotumika kuwaandaa walimu wakiwa chuoni na zile walizotumia nyanjani wakati wa mazoezi ya ufundishaji uligundua kwamba kulikuwa na tatizo katika maandalizi ya walimu. Tatizo lilikuwa kwamba mada ambazo walimu walifundishwa vyuoni hazikuwafaa walipofundisha katika shule za upili. Hivyo basi, walimu walitatizika walipowasilisha mafunzo yao wakiwa nyanjani kwenye mazoezi ya kufundisha.

Nchini Kenya, mchakato wa kuwaandaa walimu umekosolewa kwa miaka mingi. Kwa mfano, uchunguzi uliofanywa na Kamati ya Wasimamizi wa Vitivo katika Chuo kikuu cha Nairobi kuhusu kitivo cha taaluma ya elimu ulionyesha kwamba maandalizi ya walimu vyuoni yalikuwa ya kutiliwa shaka (University of Nairobi, 1978). Kufuatia ugunduzi huo, kamati hiyo ilitoa mapendekezo mawili. Kwanza, Programu ya Shahada ya Elimu ifanyiwe marekebisho ili iweze kuzingatia mahitaji ya mtalaa wa shule za upili; Pili, mafunzo ya ualimu yaandaliwe ili yaweze kumpa mwalimu umilisi wa mada zilizo katika mtalaa wa shule za upili.

Sitima (1995) anasema kuwa hata baada ya mapendekezo kutolewa na kamati ya Chuo Kikuu cha Nairobi, bado kulikuwa na matatizo katika maandalizi ya walimu katika vyuo vikuu. Sitima (1995) anafafanua udhaifu uliopo vyuoni kuhusiana na maandalizi ya walimu anaposema:

Udhaifu mkubwa unaodhihirika katika mafunzo yanayotolewa katika vyuo vikuu vinavyowaandaa walimu ni kubuni mfumo ambapo masomo makuu ambayo walimu wanaandaliwa kufundisha katika shule za upili yanafunzwa kwa kuwekwa katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

vijisehemu vidogovidogo na yanakosa kufundishwa katika njia iliyo kamilifu. Mfumo huo pia hauambatani na mada zilizomo kwenye mtalaa wa shule za upili. Kwa sababu hii, walimu hao wanapohitimu wanatatizika wanapojitahidi kufundisha baadhi ya mada ambazo hawakujifunza vyuoni ( uk. 111).

Hali anayoizungumzia Sitima (1995) inasababishwa na sera zinazobuniwa na idara za vyuo vikuu mbalimbali. Baadhi ya sera hizo huwaelekeza wanafunzi kujifunza kozi ambazo ni za lazima na zingine wanazochagua kwa hiari. Hali hii imezua taharuki kuhusu maandalizi ya walimu vyuoni na ufundishaji wao katika shule za upili hasa pale mwanafunzi anapoamua kutosoma kozi fulani, kwa mfano “Ushairi”, na ambayo huwa mada ya lazima katika mtalaa wa shule za upili.

Kutokana na yale anayoyasema Sitima (1995), changamoto zinazodhihirika katika maandalizi ya walimu vyuoni zinahusiana na malengo ya ufundishaji, mada zinazofundishwa na mfumo unaotumiwa katika uwasilishaji wa mada hizo. Kwa hivyo, kuna haja ya kuchunguza malengo ya mafunzo yanayobuniwa vyuoni kuelekeza maandalizi ya walimu ili kutathmini jinsi yanavyozingatia mahitaji ya wanafunzi. Hili linatokana na kubainika kwa changamoto zilizowakabili walimu katika kutekeleza mtalaa wa shule za upili. Isitoshe, ni muhimu pia kuzichanganua mada zilizobuniwa vyuoni kuwaandaa walimu katika kutekeleza majukumu yao shuleni ili kutambua jinsi zilivyohusiana na mada walizofundisha katika mtalaa wa Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa nchini Kenya (TUMIKE).

Kwa mujibu wa Tyler (1949), malengo ya ufundishaji yanapobuniwa ni lazima yazingatie mahitaji ya wanafunzi ili mafunzo yanayotolewa yaweze kuwafaidi. Kadhalika, Tyler anasema kuwa mada zinazobuniwa zinafaa kuwasilishwa kwa utaratibu maalumu na pia ziweze kuafiki kiwango cha wanafunzi. Hoja anazozitoa Tyler kuhusu malengo na mada zinapokiukwa, kuna uwezekano kuwa mtalaa husika unakumbwa na changamoto.

Oluoch (2006) aligundua kwamba maandalizi ya walimu wa shule za upili nchini Kenya yalikumbwa na changamoto nyingi. Moja kati ya changamoto hizo ni matumizi ya mfumo wa ufundishaji alioutaja Sitima (1995). Changamoto nyingine aliyoitambua ilihusiana na mitalaa iliyotumiwa vyuoni. Oluoch (2006) alieleza kwamba mitalaa hiyo ilikuwa mipana kwa kuwa ilikuwa na mada nyingi na haikuwezekana kuzifundisha zote kwa muda ambao ulibainishwa katika mihula na miaka mbalimbali ya masomo vyuoni. Hali hii ilisababisha baadhi ya mada hizo kutofundishwa na kuwafanya walimu kutopata maandalizi ya kina. Kuhusiana na wingi wa mada, Tyler (1949) anaeleza kuwa idadi ya mada katika mtalaa iwe ile ambayo mwalimu anaweza kumudu kufunza kikamilifu kulingana na kipindi cha mafunzo. Ugunduzi wa Oluoch (2006) unachochea kuchunguzwa kwa mada zinazofundishwa vyuoni ili kutathmini wingi na upana wake na uchangamano unaotokea mada hizo zinapowasilishwa.

Isitoshe, kwa mujibu wa Oluoch (2006), changamoto nyingine iliyokumba maandalizi ya walimu ilitokana na namna tathmini ilivyofanyika katika vyuo vikuu. Kwa mujibu wa Tyler (1949), tathmini inapofanyika, inalenga kukadiria ufanisi wa kufikiwa kwa malengo ya elimu kupitia ufundishaji wa mada zilizo kwenye mtalaa. Matokeo ya tathmini yanatarajiwa kubainisha ubora na udhaifu wa mfumo wa elimu. Kufuatia hoja hii, tathmini inayofanyika vyuoni inatarajiwa kufichua changamoto zinazokumba utekelezaji wa mitalaa. Hata hivyo, Oluoch (2006) anasema hili halijabainika kwa sababu ya mfumo wa ukadiriaji unaotumika vyuoni. Oluoch anaendelea kusema kuwa tathmini inayofanyika vyuoni inadhibitiwa na wahadhiri ambao ndio watekelezaji wa mitalaa. Kwa kuwa wao hudhibiti mfumo wa tathmini, inawezekana wao kuandaa tathmini inayotarajiwa kutimiza maslahi yao na wala siyo maslahi ya wanafunzi. Tyler (1949) anahimiza kuwa mfumo mzuri wa tathmini husisitiza kuwepo kwa ukadiriaji wa mara kwa mara. Kufuatia ugunduzi wa Oluoch (2006) pana haja ya kuchunguza mfumo wa tathmini unaotumika katika vyuo vikuu ili kutambua jinsi unavyotumika kukadiria ufanisi wa malengo ya ufundishaji, ufaafu wa mada zinazofundishwa vyuoni na jinsi zinavyowasilishwa.

Hali nyingine ambayo inaweza kuathiri maandalizi ya walimu vyuoni ni ule upekee wa kila chuo katika kubuni sera mbalimbali ambazo zinadhibiti mafunzo yanayotolewa kwa walimu. Japo mitalaa inayotumiwa kuwaandaa walimu katika vyuo vikuu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

mbalimbali ina vipengele vya kimsingi vinavyoshabihiana, utekelezaji wa mitalaa hiyo hutofautiana kutoka chuo kimoja hadi kingine. Tofauti hujitokeza kupitia kwa sera zinazohusu masuala kama vile idadi ya kozi ambazo wanafunzi wanastahili kujifunza wanapokuwa vyuoni; kozi za hiari na za lazima; na vipindi (mihula na miaka) mahsusi ambapo kozi hizo zinaporatibiwa kufundishwa. Wanafunzi wanapojiunga na vyuo vikuu mbalimbali hutarajiwa kuzingatia sera zinazoelekeza mafunzo wanayopokea. Kwa kuwa kila chuo kina sera zake, ni bayana kuwa mada zilizo katika mitalaa ya vyuo vikuu hutekelezwa kwa namna tofauti. Hali hii inaibua shaka kwa kuwa walimu hao wanatarajiwa kutekeleza mtalaa mmoja wa shule za upili hata ingawa wameandaliwa kwa namna tofauti.

Hali iliyorejelewa na Sitima (1995) na Oluoch (2006) ilisababishwa na ugumu wa vyuo vikuu nchini Kenya kutekeleza mabadiliko katika mipangilio yake na mikakati ya ufundishaji. Suala hili limejadiliwa na Kafu (2013) na kusisitizwa na Nasimiyu (2017). Wataalamu hawa wanasema kuwa ingawa mabadiliko yanatokea katika jamii, vyuo vikuu vingi nchini Kenya havifanyi marekebisho ambayo hunuia kuimarisha utendakazi wake.

Kutokana na maoni mbalimbali (Taz. UoN, 1978; Sitima, 1995; Oluoch, 2006; Kafu, 2013 & Nasimiyu; 2017) maandalizi ya walimu wa shule za upili nchini Kenya yanakumbwa na changamoto kuu nne: upana na uteuzi wa mada; malengo ya mafunzo ya Kiswahili kutegemea kila chuo kikuu; mfumo wa ufundishaji wa kozi za Kiswahili vyuoni; na mfumo wa tathmini unaotumiwa na walimu wa vyuo vikuu.

Kwa upande mwingine, walimu wa Kiswahili katika shule za upili hutarajiwa kufundisha mada maalumu ambazo zimeteuliwa na kuratibiwa na TUMIKE. Pia walimu hao hufundisha kwa kuongozwa na malengo maalumu. Aidha, walimu wa Kiswahili katika shule za upili hufuata njia, mbinu na mikakati iliyopendekezwa na TUMIKE. Vilevile, tathmini ya Kiswahili katika shule zote za upili hufanyika kwa njia maalumu zinazofanana.

Ni kutokana na hali hizi katika mitalaa ya vyuo vikuu na mtalaa wa TUMIKE katika shule za upili ambapo utafiti huu ulifanywa ili kutathmini utekelezaji wa mitalaa rasmi ya Kiswahili katika vyuo vikuu. Utafiti pia ulinuia kuchunguza namna ambavyo utekelezaji wa mitalaa katika vyuo vikuu uliathiri utendakazi wa walimu wa shule za upili walipofundisha yaliyomo katika mtalaa wa TUMIKE.

**Suala la Utafiti**

Maoni mbalimbali yametolewa kuhusu changamoto za maandalizi ya walimu vyuoni na utekelezaji wa majukumu yao shuleni (Taz. UoN,1978; Sitima, 1995; Oluoch, 2006; Kafu, 2013 & Nasimiyu, 2017). Miongoni mwa masuala yanayojitokeza katika utafiti wa wataalamu hawa mbalimbali ni pamoja na changamoto zinazohusu malengo, mada, utekelezaji na tathmini ya mitalaa. Utafiti mchache umefanywa kuhusu maandalizi ya walimu wa Kiswahili (Mbuthia, 1996 & Wagari, 2003). Hata hivyo, haijapambanuliwa ni kwa namna gani maandalizi hayo yanaathiri utendakazi wao darasani. Kadhalika, utafiti wa kina haujafanywa kuchunguza namna ambavyo vipengele vya mtalaa (malengo, mada, utekelezaji na tathmini) vinahusiana na kuathiri suala zima la maandalizi ya walimu wa Kiswahili na athari zake kwa utendakazi wao baada ya wao kuhitimu. Shaka inaibuka ambapo vyuo vikuu vinawaandaa walimu kwa kutumia mitalaa tofauti ilhali wanatarajiwa kufundisha mtalaa mmoja katika shule za upili nchini Kenya. Ni kutokana na hali hii ndipo utafiti huu ulinuia kutathmini namna utekelezaji wa mitalaa ya Kiswahili katika vyuo vikuu uliathiri utendakazi wa walimu walipotekeleza mtalaa wa Kiswahili unaoandaliwa na TUMIKE kwa ajili ya shule za upili nchini.

**Malengo ya Utafiti**

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kutathmini uhusiano uliopo baina ya mitalaa ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya umma na mtalaa wa Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Utafiti ulilenga kuonyesha hali halisi iliyopo baina ya maandalizi ya walimu wa Kiswahili katika vyuo vikuu vya umma na namna wanavyotekeleza mtalaa ulioundwa na TUMIKE kwa ajili ya kufundishwa katika shule za upili. Utafiti ulikusudia kufikia madhumuni mahususi yafuatayo;

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

- Kupambanua vipengele vinavyounda mitalaa ya Kiswahili inayotumika katika vyuo vikuu vya umma na vipengele vilivyo katika mtalaa wa Kiswahili wa shule za upili nchini Kenya.

- Kujadili namna ambavyo vipengele vya mtalaa huathiri utekelezaji wake katika vyuo vikuu na utendakazi wa walimu wa shule za upili wanapotekeleza mtalaa wa Kiswahili ulioandaliwa na TUMIKE.

## UHAKIKI WA MAANDISHI

### Dhana ya Mtalaa

Dhana ya mtalaa ni changamano kwa kuwa imefasiriwa kwa namna mbalimbali na wataalamu tofauti (Taz. Bobbit,1918; Tyler,1949; Taba,1962; Oliver,1982; Shiundu & Omulando,1992 & Oluoch,2006). Maelezo yaliyotolewa na wataalamu hawa yanadhihirisha kuwa mtalaa unahusu kinachotarajiwa kufanyika na namna kinavyostahili kutendeka katika mfumo wa elimu. Fasiri za wataalamu hawa zinaonyesha kuwa mtalaa ni mfumo, mchakato, mpangilio maalumu wa shughuli katika mfumo wa elimu na pia ni nyaraka maalumu zilizoandikwa kuonyesha vipengele vinavyoelekeza mfumo wa elimu.

Japo kuna aina tatu za mitalaa, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mtalaa rasmi. Mtalaa rasmi umefafanuliwa na Urevbu (1985) kuwa ni jumla ya mambo ambayo wanafunzi hufundishwa shuleni na yameorodheshwa katika silabasi. Shiundu & Omulando (1992) na Oluoch (2006) wanasema mtalaa rasmi unahusisha jumla ya mambo yaliyoorodheshwa katika silabasi ambayo huonyesha malengo, mada, njia za kufundisha, mifumo ya ukadiriaji na nyenzo za ufundishaji.

Maelezo yaliyotolewa na wataalamu tofauti kuhusu mtalaa rasmi yanaonyesha kuwa unajumlisha vipengele vinne vikuu: malengo, mada, utekelezaji na tathmini. UNESCO (2011) inaeleza kuwa mwalimu anayo nafasi muhimu katika utekelezaji wa mtalaa rasmi kwa kuwa ndiye anayewasilisha yaliyopangwa kwa kuratibu shughuli za ufundishaji darasani, kubuni njia, mikakati na nyenzo za ufundishaji pamoja na kuchagua mbinu za ukadiriaji zinazowasaidia wanafunzi kufikia malengo ya ujifunzaji wao.

Utafiti ulikusudia kuchunguza vipengele vinavyounda mitalaa ya Kiswahili ya vyuo vikuu na mtalaa wa shule za upili ulioundwa na TUMIKE na jinsi ambavyo vipengele hivi vinaathiri utekelezaji wake katika vyuo vikuu na utendakazi wa walimu katika shule za upili. Katika utafiti alioufanya kuhusu vipengele vya mtalaa rasmi, Brown (1995) anaeleza kwamba kabla ya kuanzisha mafunzo yake, ni muhimu kwa walimu ambao ni watekelezaji wa mtalaa kutambua vipengele vinavyouunda, kuvifasiri na kuvifafanua kwa kina. Baadaye, wavitathmini kabla ya kuanza shughuli ya mafunzo, mafunzo yanapoendelea na baada ya mafunzo kukamilika. Hili hufanyika ili kutathmini nafasi ya kila kipengele katika utekelezaji wa mtalaa.

### Malengo ya Utekelezaji wa Mtalaa Rasmi

Kwa mujibu wa Tyler (1949), malengo ya mtalaa ni kauli ambazo hufafanua mabadiliko ya kitabia yanayotarajiwa kutokea miongoni mwa wanafunzi baada ya kupokea mafunzo. Malengo ni muhimu kwa mwalimu anapotekeleza mtalaa kwa kuwa humwezesha kubaini stadi na maarifa mahususi ambayo mwanafunzi hutarajiwa kupata kutokana na mafunzo anayopokea (Brown,1995). Malengo haya ndiyo huelekeza shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwa ni kupitia kwa shughuli ya ufundishaji ndipo yanafikiwa.

Utafiti ulikusudia kutambua namna malengo ya ufundishaji katika vyuo vikuu yalifikiwa. Kufikiwa kwayo kulithibitishwa kupitia kwa utendaji wa walimu wa shule za upili walipotekeleza mtalaa wa TUMIKE katika shule za upili. Tyler (1949) alibaini kuwa malengo ya mtalaa yalibuniwa kutokana na mahitaji ya wanafunzi, jamii na wataalamu. Utafiti ulikusudia kutambua namna ambavyo hali hii ilidhihirika katika malengo ya mitalaa vyuoni na shuleni.

Utafiti uliofanywa na Musau (2002) ulionyesha kwamba mitalaa ya Kiswahili katika vyuo vikuu inakosolewa kwa kutokidhi mahitaji ya wanafunzi kwa kuwa ina mwegemeo wa kinadharia ambao hauruhusu ujifunzaji wa lugha kwa viwango vya juu kama ilivyo katika lugha za kimataifa. Anaendelea kusema mitalaa inayotumiwa vyuoni hutegemea tajiriba na hisia za wahadhiri kuhusiana na lugha

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

hivyo basi haijafikia viwango vinavyohitajika na pia haizingatii mahitaji ya wanafunzi.

Simala (2002), katika utafiti alioufanya kuhusu mitalaa inayotumika vyuoni aligundua kuwa mitalaa vyuoni ni ya kimapokeo na kwamba wahadhiri hawaruhusiwi kufundisha kozi walizobobea kwa ubunifu na utaalamu unaohitajika. Alipendekeza kuwe na mabadiliko ya mara kwa mara ya mitalaa hiyo ili iweze kukidhi mahitaji ya jamii na yale ya wanafunzi.

Katika utafiti wake, King'ei (2001) alibainisha malengo ya kijumla yaliyobuniwa ili kutelekeza ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu vyote. Naye Adegoke (2010) alibainisha malengo mahususi yanayofaa kutelekeza maandalizi ya walimu katika vyuo vikuu. Utafiti huu umelenga kuchunguza malengo yaliyobuniwa katika vyuo vikuu mbalimbali vya umma kwa ajili ya kuwaandaa walimu wa Kiswahili ili kubaini iwapo yalifikia mahitaji yao kama wanafunzi walioandaliwa ili kuutekeleza mtalaa ulioandaliwa na TUMIKE kutekelezwa katika shule za upili.

**Mada katika mitalaa rasmi**

Mada ni jumla ya stadi zinazofundishwa katika asasi za elimu (Bilbao n.w, 2008). Mada hizi huwasilishwa kama masomo mahsusi na hutarajiwa kuwa ufundishaji wa mada hizi utasababisha mabadiliko ya kitabia miongoni mwa wanafunzi na jamii kwa jumla. Kwa mujibu wa Adegoke (2010) na Hedge (2002), kubuniwa kwa malengo ya ufundishaji huamua uteuzi wa mada zinazofundishwa. Flowerdiew na Peacock (2001) wanasema ufundishaji mzuri wa mada hutokea iwapo walimu watakuwa na ufahamu wa kina kuhusu wanachotarajiwa kufundisha, maarifa kuhusu njia za ufundishaji na mabadiliko ya kitabia yanayotarajiwa kutokea miongoni mwa wanafunzi. Utafiti ulikusudia kuchunguza namna ambavyo uteuzi wa mada zilizofundishwa vyuoni ziliwaandaa walimu kuwasilisha mada katika mtalaa wa TUMIKE ulioandaliwa ili upate kutekelezwa katika shule za upili.

**Utekelezaji wa mitalaa rasmi**

MacArthur na Baron (1983) wanasema kuwa mwalimu aliyeandaliwa vyema anaweza kutegemewa katika kuutekeleza mtalaa. Kwa mujibu wa Oyedeji (1998), lengo kuu la kuutekeleza mtalaa ni kuhakikisha kuwa ujifunzaji umetokea miongoni mwa wanafunzi. Hili huweza kufikiwa iwapo kutabuniwa mbinu bora za kufundisha katika viwango vyote vya elimu (Makoti, 2017).

Simala (2019) anaeleza kuhusu umuhimu wa kuwapa walimu mafunzo bora ikiwa watategemewa katika kutekeleza mitalaa ipasavyo. Anasema kuwa taratibu zinazozingatiwa na walimu katika utekelezaji wa mitalaa huhitaji mafunzo ya hali ya juu. Kwa hivyo, walimu walioandaliwa vyema wanao ujuzi wa kutekeleza mtalaa uliopo ili kuwapa wanafunzi ujuzi wa kukabiliana na hali mbalimbali za maisha.

Utekelezaji wa mtalaa hutegemea mikabala, mbinu na njia mbalimbali za ufundishaji. Uchunguzi uliofanywa na Mutiga (2008) kuhusu ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili uligundua kuwa ufundishaji wake ulikumbwa na matatizo kutokana na mikabala iliyotumika ambayo ilipelekea wanafunzi kukariri mafunzo waliyopokea bila kupata umilisi na ufahamu wa lugha uliokusudiwa. Mafunzo yaliyotolewa yaliwezesha wanafunzi kupita mitihani wala siyo kupata umilisi wa lugha. Alipendekeza matumizi ya mikabala kadhaa ambayo ingewasaidia wanafunzi kupata umilisi wa mada na stadi za lugha kupitia mafunzo ambayo yangewawezesha kumudu mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.

Utafiti uliofanywa na Asiimwe (2019) kuhusu mikabala ya kufunza sarufi ya Kiswahili katika vyuo vikuu uligundua kuwa wahadhiri walitumia mikabala ya kale iliyochakaa. Alipendekeza matumizi ya mikabala ya kisasa inayodhaniwa kuwa bora hasa mkabala wa kimawasiliano katika ufundishaji wa sarufi ya Kiswahili.

Makoti (2017) alipofanya uchunguzi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu aligundua kwamba ulikumbwa na changamoto kwa kuwa haukutekelezwa ilivyostahili. Hali hii ilitokana na matumizi ya mikabala isiyofaa katika kuwasilisha mada kwenye mitalaa. Alipendekeza matumizi ya mitalaa ifaayo.

Tafiti zilizofanywa na Eshiwani (1993); Musungu na Nasongo (2008): Mutiga (2008), Otunga (2010) na Makoti (2017) kuhusu ufundishaji katika shule za upili ulionyesha kwamba mikabala iliyotumika

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

haikuwezesha mwanafunzi kupata umilisi wa yale aliyojifunza mtalaa ulipotekelezwa.

Njia za ufundishaji zina nafasi kubwa katika utekelezaji wa mitalaa shuleni na vyuoni. Eisner (2002) anasema kuwa uwasilishaji bora wa mitalaa hutegemea sana njia zinazotumiwa na mwalimu. Naye Adegoke (2010) aligundua kuwa walimu walipoutekeleza mtalaa kwa kutumia njia zilizohusisha utendaji wa mwanafunzi, mwanafunzi aliweza kushika mafunzo haraka na kuyahifadhi katika kumbukumbu kwa muda mrefu kuliko njia zilizompa mwalimu nafasi kuu ya utendaji.

Tyler (1949) anasisitiza matumizi ya njia zinazompa mwanafunzi nafasi kuu ili ajigundulie mambo na pia aweze kujitegemea pasipo kumtegemea mwalimu kwa kiwango kikubwa. Utafiti ulilenga kuchunguza namna ambavyo njia za ufundishaji zinazotumiwa vyuoni kuwaandaa walimu ziliathiri utendakazi wao walipoutekeleza mtalaa wa Kiswahili katika shule za upili.

## Tathmini ya Mitalaa

Tyler (1949) anaeleza tathmini kuwa ni mchakato unaolenga kupima namna ambavyo malengo ya mtalaa rasmi yalivyoafikiwa katika mfumo wa elimu kupitia kwa mafunzo yanayotolewa. Tathmini hupima kiwango cha mabadiliko ya kitabia yanayotarajiwa kutokea miongoni mwa wanafunzi baada ya wao kupokea mafunzo.

Simala (2019) anasema kuwa tathmini ya mitalaa ni muhimu kwa kuwa huwachochea walimu na wanafunzi kutia bidii katika ufundishaji na ujifunzaji wao. Anaendelea kusema kuwa tathmini bora hupima alichofunza mwalimu siyo alichojifunza mwanafunzi.

Matokeo ya tathmini hutumika kuimarisha utekelezaji wa mitalaa katika asasi za elimu kwa kuwa ni njia moja inayotumika kupima utekelezaji bora wa mitalaa. Isitoshe, tathmini hupima kufikiwa kwa malengo ya mtalaa ambapo matokeo yake huamua pia ubora wa mada zilizoteuliwa. Utafiti ulinuia kuchunguza jinsi ambavyo mifumo ya tathmini vyuoni iliathiri utekelezaji wa mtalaa katika shule za upili.

## NJIA ZA UTAFITI

Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa usoroveya elezi ambapo data ilikusanywa kutoka nyanjani kwa walimu wa Kiswahili wa shule za upili, wahadhiri wa Kiswahili katika vyuo vikuu vya umma pamoja na wasimamizi wa idara za Kiswahili katika vyuo vikuu vya umma.

Jumla ya shule za upili 42 kutoka katika Kaunti ya Bungoma zilitumika katika utafiti huu. Ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi sampuli nasibu ya uratibu kati ya jumla ya shule 140 zilizo katika Kaunti hii. Shule hizo 42 zilikuwa ni asilimia 30 ya shule zote 140. Walimu wa Kiswahili 42 wa Kiswahili wa shule za upili waliteuliwa kupitia kwa mbinu ya uteuzi sampuli sahili nasibu. Wahadhiri wa somo la Kiswahili 17 kutoka katika vyuo vikuu vya umma nchini Kenya waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi sampuli sahili nasibu. Hawa 17 walikuwa ni asilimia 30 ya jumla ya idadi ya wahadhiri wote wa somo la Kiswahili kutoka katika kila chuo kikuu kati ya vile vyuo vikuu 5 vya umma vilivyoteuliwa kwa mbinu ya uteuzi sampuli kimaksudi. Wasimamizi wa idara za Kiswahili 5 waliteuliwa kutoka katika vyuo vikuu vya umma husika. Hawa waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi sampuli kimaksudi kwa kuwa walilengwa moja kwa moja.

Data ilikusanywa kwa kutumia njia tatu kuu: hojaji, usaili na uchanganuzi wa nyaraka. Hojaji iliandaliwa kwa ajili ya walimu wa Kiswahili katika shule za upili na wahadhiri wa somo la Kiswahili katika vyuo vikuu vya umma. Kupitia kwa hojaji, walimu na wahadhiri walitoa habari kuhusu; mtalaa rasmi wa TUMIKE, mitalaa inayotumika kufundisha katika vyuo vikuu, vipengele vinavyounda mitalaa hiyo na changamoto zilizokumba utekelezaji wa mitalaa ya Kiswahili katika shule za upili na vyuo vikuu vya umma. Hojaji ya walimu wa shule za upili pia ililenga kutathmini namna ambavyo utekelezaji wa mitalaa rasmi vyuoni iliathiri utendakazi wao shuleni. Usaili ulilenga wasimamizi wa idara za Kiswahili vyuoni na walitarajiwa kutoa habari kuhusu mitalaa ya Kiswahili iliyotumiwa vyuoni, vipengele vyake, namna ilivyotekelezwa na changamoto zilizokumba utekelezaji wake.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

Nyaraka zilizochanganuliwa zilikuwa na habari mahsusi kuhusu mitalaa rasmi iliyotumiwa shuleni na vyuoni. Baadhi ya nyaraka zilizochanganuliwa ni; silabasi ya Kiswahili ya shule za upili; miongozo ya kozi za Kiswahili zilizofundishwa katika vyuo vikuu 5 vya umma vilivyoteuliwa; maandiko yanayotoa ufafanuzi kuhusu kozi hizo. Zilichanganuliwa ili kupata data kuhusu vipengele vya mitalaa (malengo, mada, njia za utekelezaji na mifumo ya tathmini).

Mrejesho kutoka kwa watafitiwa uliwezesha utafiti kubaini namna ambavyo mitalaa rasmi ya Kiswahili ilivyotekelezwa katika vyuo vikuu vya umma na shule za upili kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya mtalaa. Isitoshe, mrejesho pia uliwezesha kubaini namna ambavyo utekelezaji wa mitalaa ya Kiswahili katika vyuo vikuu uliathiri utendakazi wa walimu wanaofundisha katika shule za upili.

## UCHANGANUZI NA MATOKEO

Data iliyokusanywa katika utafiti huu ilichanganuliwa kwa njia mbili kuu; njia ya kimaelezo na ile ya kitakwimu. Data iliyokusanywa kutokana na usaili, hojaji na uchanganuzi wa nyaraka ilichanganuliwa kimaelezo. Data iliyokusanywa kutokana na hojaji funge ilichanganuliwa kitakwimu. Uchanganuzi wa kimaelezo na kitakwimu uliwezesha utafiti kushughulikia data iliyokusanywa kwa njia maalumu ili kupata matokeo yaliyohusiana na suala la utafiti. Data iliyochanganuliwa ilihusu vipengele vikuu vya mitalaa ambavyo ni malengo, mada, utekelezaji na tathmini.

### Malengo ya mitalaa

Utafiti uligundua kuwa Progamu ya Shahada ya Elimu katika kila chuo kikuu ilibainisha lengo moja la kijumla. Ilitarajiwa kwamba malengo mengine mahsusi ambayo yalilenga maandalizi ya walimu yangebuniwa kutokana na lengo hilo moja. Hilo halikutokea. Hata hivyo, katika baadhi ya vyuo vikuu kama vile Masinde Muliro, Moi na Nairobi, malengo ya programu ya Shahada ya Elimu yalifafanua kuwa vyuo hivyo viliandaa walimu wa shule za upili lakini vyuo vikuu vya Kenyatta na Egerton vililenga kuandaa walimu wa shule za upili, wasimamizi wa taasisi za elimu, waandalizi wa sera katika sekta ya elimu na wasimamizi wa masuala ya elimu katika wizara ya elimu. Hali ya baadhi ya vyuo vikuu kubuni malengo sawa ya kuandaa walimu wa shule za upili na wasimamizi katika sekta zingine zinazohusu masuala ya elimu kama vile wizara ya elimu inaweza kuwa inachangia kutobuniwa kwa malengo mahsusi ya kuwaandaa walimu. Kuna uwezekano mkubwa kuwa hali hii imeathiri namna ambavyo walimu hawa wanaandaliwa na hatimaye kutekeleza mtalaa wa TUMIKE katika shule za upili.

Katika baadhi ya vyuo vikuu kama Moi, Kenyatta na Nairobi ambako kulikuwa na Shahada ya Sanaa ya Kiswahili, wahadhiri waliowaandaa walimu wa Kiswahili ndio wale wale waliowaandaa wanataaluma wa Kiswahili kupitia kwa Programu ya Shahada ya Sanaa ya Kiswahili. Hali hii ilipelekea wahadhiri hao kubuni malengo ya kijumla yaliyoelekeza ufundishaji wa programu hizi mbili. Malengo hayo ya kijumla yalitumiwa kuandaa walimu na wanataaluma ya Kiswahili. Kuwepo kwa malengo ya kijumla ya kuwaandaa walimu wa shule za upili kunaathiri maandalizi pamoja na utendakazi wao katika shule za upili. Ndio maana kuna haja ya kutenganisha programu hizi mbili pamoja na wahadhiri wanaozifunza ili wahadhiri wanaowaandaa walimu wabainike na wabuni malengo mahususi ya kuwaandaa walimu.

Utafiti huu uligundua kuwa wahadhiri waliowaandaa walimu katika vyuo vikuu walielekezwa na malengo ya kufunza kozi mbalimbali ambayo yaliwasaidia wanafunzi kuwasilisha mada zilizo katika kozi walipohitimu kuwa walimu. Malengo ya kozi hayakuwa ya kuwaandaa kuwa walimu. Hata hivyo, malengo ya kozi yalikuwa mahsusi, yaliweza kupimika na yaligawika katika viwango vitatu; maarifa, utendaji na hisia.

Japo malengo ya mitalaa ya vyuo vikuu yalihusiana kwa karibu na yale ya shule za upili kisifa na hasa kwa kuzingatia kielelezo cha Tyler, malengo ya kufundisha vyuoni yalibuniwa vyuoni katika idara husika ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi katika vyuo mahsusi. Kila chuo kikuu kilibuni malengo yake. Kwa upande mwingine, malengo ya kufundisha katika shule za upili yalibuniwa na TUMIKE ili yatumiwe katika shule zote nchini. Kwa hivyo malengo ya mtalaa rasmi wa shule za upili yalisawazishwa kote nchini lakini ya vyuo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

vikuu yalitofautiana. Kutofautiana kwa malengo ya mitalaa rasmi iliyobuniwa katika vyuo vikuu mbalimbali iliyowaandaa walimu kuliathiri namna walimu hawa walivyofundishwa kwa kuwa waliandaliwa kwa namna tofauti pia.

Mitalaa ya vyuo vikuu ni changamano kwa kuwa kila chuo kina programu zake zinazokitofautisha na vyuo vingine ikikumbukwa kuwa vyuo vikuu vya umma vilianzishwa kwa misingi tofauti. Hata hivyo, kwa kuwa vyuo vikuu huwaandaa walimu wa shule za upili kutekeleza mtalaa mmoja ulioandaliwa na TUMIKE, kuna haja ya kusawazisha pia malengo ya mitalaa rasmi inayotumiwa kuwaandaa vyuoni. Tume ya elimu ya vyuo vikuu inaweza kutoa mwongozo kuhusu hili ili kubuniwe sera madhubuti katika vyuo vikuu zinazoelekeza maandalizi ya walimu wa shule za upili katika vyuo vikuu vyote. Hali hii itasawazisha namna wanavyotekeleza mtalaa rasmi ulioandaliwa na TUMIKE kutekelezwa katika shule za upili.

**Mada katika Mitalaa**

Mada katika mitalaa ya vyuo vikuu zimeorodheshwa katika kozi mbalimbali. Mada zilizoorodheshwa kwenye kozi ndizo huunda silabasi zinazotumika katika vyuo vikuu. Kozi zilibuniwa katika idara na kuidhinishwa na kamati ya vitivo mbalimbali kisha baadaye seneti. Hata hivyo, mada katika kozi ambazo huunda silabasi hubuniwa na wahadhiri na kuidhinishwa katika idara.

Kuna kozi za hiari na za lazima katika vyuo vikuu vyote japo kuna hali ambapo kozi inaweza kuwa ya hiari katika chuo kimoja na ikawa ya lazima katika chuo kingine. Kwa ujumla, kozi za lazima zilikuwa nyingi kuliko za hiari. Mada katika kozi hizi ziligawika katika mikondo mitatu ambayo ni: fasihi, lugha na isimu. Kati ya hii mikondo mitatu, kozi zilizokuwa na mada za fasihi zilikuwa nyingi zikifuatiwa na za lugha na hatimaye za isimu. Kila chuo kikuu kilikuwa na idadi maalumu ya kozi zilizokuwa na mada za mikondo yote mitatu. Utafiti uligundua kuwa kozi za isimu ni chache sana vyuoni. Hali hii iliathiri namna walimu hawa walitekeleza mtalaa wa TUMIKE kwa kuwa walipohojiwa walisema walipendelea kufunza mada za fasihi na walipata ugumu katika kuwasilisha mada za lugha ambazo zilijumlisha sarufi na isimu. Hali hii ilisababishwa na vyuo kufunza kozi chache za isimu na lugha. Vyuo vikuu vinashauriwa kuzidisha idadi ya kozi za isimu na lugha ili kuimarisha ufundishaji wa lugha katika shule za upili ikikumbukwa kuwa moja kati ya malengo ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili ni kumwezesha mwanafunzi kuwasiliana vyema kwa lugha hii. Lugha na isimu hufunza kuhusu sheria za lugha ambazo mwanafunzi anapozimilisi, atakuwa na mbinu nzuri za mawasiliano. Kwa sababu hii, kuna haja ya kuimarisha ufundishaji wa lugha na isimu vyuoni.

Kuna hali zilizotofautisha ufundishaji wa mada katika mtalaa rasmi wa shule za upili na mitalaa ya vyuo vikuu. Katika mtalaa wa TUMIKE, wanafunzi walitarajiwa kujifunza mada zote zilizoorodheshwa katika silabasi ilhali katika vyuo vikuu, wanafunzi walikuwa huru kuchagua baadhi ya mada kwa hiari japo kulikuwa na mada zilizokuwa za lazima. Uchaguzi wa mada za hiari na lazima ulitofautiana kutoka chuo kimoja hadi kingine. Hali hii iliibuka kuwa suala changamano kwa kuwa walimu kutoka vyuo vikuu tofauti walikojifunza kozi za lazima na hiari huku walitarajiwa kufunza mada zote katika mtalaa wa TUMIKE hata zile ambazo hawakujifunza vyuoni. Hali hii iliathiri utendakazi wao walipofundisha katika shule za upili. Walimu walisema kuwa ilikuwa rahisi kwao kufundisha mada walizojifunza vyuoni kuliko ilivyokuwa kwao kuwasilisha mada ambazo hawakujifunza kwa kuwa zilifanywa kuwa za hiari vyuoni walikosomea.

Tofauti zinazojitokeza kati ya mada katika mitalaa yote miwili na namna zinavyoshughulikiwa ni hali inayoibua maswali. Kwa mfano, ni vipi walimu wa shule za upili watafundisha mada zilizo katika silabasi ya TUMIKE ikiwa hawakujifunza kozi zilizoorodhesha mada hizo vyuoni hasa ikiwa zilikuwa ni kozi za hiari? Hii ni changamoto ambayo ilihitaji kushughulikiwa kwa kuwa inaathiri utendakazi wa walimu hawa wanapoutekeleza mtalaa wa TUMIKE jinsi ilivyoelezwa hapo awali. Ingekuwa vyema iwapo kozi zilizokuwa na mada zilizofundishwa katika shule za upili zingefanywa kuwa za lazima katika vyuo vikuu vyote. Hili likifanyika, walimu watautekeleza mtalaa wa shule za upili kwa njia bora itakayoimarisha ufundishaji wa Kiswahili nchini.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

### Utekelezaji wa Mitalaa

Utekelezaji wa mitalaa rasmi katika vyuo vikuu na shule za upili uliwategemea walimu na wahadhiri. Wao ndio walidhibiti utekelezaji wa mitalaa rasmi kwa kuwa waliamua mikabala, njia za ufundishaji, mikakati, mbinu na nyenzo zilizostahili kutumika.

Wahadhiri waliotekeleza mitalaa katika vyuo vikuu walipata mafunzo ya kitaaluma vyuoni walikopata shahada yao ya kwanza. Wengi wao walikuwa na shahada ya elimu japo kuna wachache ambao hawakupata mafunzo ya ualimu, shahada yao ya kwanza ilikuwa ni ya Sanaa katika somo la Kiswahili. Kuna uwezekano kuwa wahadhiri waliokuwa na Shahada ya Sanaa walipotekeleza mitalaa ya vyuo vikuu nchini kuwaandaa walimu, waliongozwa na malengo ya kijumla ya ufundishaji wa somo la Kiswahili kulingana na jinsi walivyoandaliwa. Hawakuelekezwa na malengo ya kuwaandaa walimu wa shule za upili jinsi walivyofanya wahadhiri ambao shahada yao ya kwanza ilikuwa ya ualimu. Kwa hivyo maandalizi ya walimu vyuoni yalitegemea wahadhiri waliowasilisha yaliyomo kwenye mitalaa iliyotumiwa kuwaandaa.

Wahadhiri walipowaandaa walimu vyuoni waliongozwa na mikabala na njia mbalimbali za ufundishaji. Utafiti uligundua kuwa mkabala walioutumia zaidi ni ule wa ukadiriaji. Ingawa huu ndio mkabala unaojitokeza katika kielelezo cha Tyler, umekosolewa kwa kuwa unaegemea sana upitaji wa mitihani kuliko umilisi wa maarifa ambao wanafunzi walitarajiwa kuupata kutokana na mafunzo waliyopokea vyuoni. Je, inawezekana kuwa mikabala iliyoelekeza maandalizi ya walimu vyuoni iliathiri utendakazi wao shuleni? Waliathiriwa kwa kiwango kikubwa kwa kuwa hata wao katika utendakazi wao walikadiria ufahamu wa wanafunzi wao kupitia kwa mitihani. Alama ambazo wanafunzi walipata katika mitihani na mijarabu yao ilitumiwa kama kigezo kilichoamua ubora wa walimu na wanafunzi. Hata hivyo, mikabala inayopendekezwa na wataalamu wa masuala ya lugha ni ile inayohimiza utendaji miongoni mwa wanafunzi na wala siyo ile inayolipa suala la ukadiriaji kipaumbele.

Njia na mikabala iliyotumiwa vyuoni kuwaandaa walimu iliathiri pakubwa utendakazi wao kwa kuwa mwanafunzi huathiriwa kwa kiwango kikubwa na mwalimu wake. Ndio maana njia za ufundishaji zilizotumiwa katika kutekeleza mitalaa vyuoni na shuleni zilisetwa zikawa ni zile zilizompa mwanafunzi nafasi kuu na zile zilizompa mwalimu nafasi kuu. Njia za aina zote mbili zilichangiana na kufidiana. Utafiti uligundua kuwa wahadhiri na walimu walichagua njia za ufundishaji kwa kuongozwa na mada walizowasilishwa, kiwango cha wanafunzi na malengo waliyotaraji kuafikia.

Iligunduliwa kupitia kwa utafiti kuwa utekelezaji wa mitalaa rasmi ya Kiswahili vyuoni uliathiri ule wa shuleni kwa kuwa walimu na wahadhiri walitumia mikabala, njia, mbinu na nyenzo kwa namna moja. Hata hivyo, katika kutekeleza mitalaa vyuoni, wahadhiri hawakudhibitiwa jinsi walimu wa shule za upili walivyodhibitiwa na washikadau mbalimbali. Hali hii ya kutodhibitiwa ilisababisha ulegevu wa kiwango fulani miongoni mwa wahadhiri hali ambayo iliathiri maandalizi ya walimu. Iwapo kungekuwa na njia ya kukadiria utendakazi wa walimu waliohitimu kutoka vyuo vikuu mbalimbali, huenda ulegevu uliopo katika utekelezaji wa mitalaa rasmi vyuoni ungegunduliwa na kukabiliwa vilivyo.

### Tathmini ya Mitalaa

Mitalaa rasmi ya vyuo vikuu na shule za upili ilifanyiwa tathmini katika viwango na nyakati tofauti. Tathmini ilifanyika ili; kupima jinsi malengo ya ufundishaji yalikuwa yamefikiwa, kukadiria kiwango cha mafunzo yaliyotolewa kwa wanafunzi, kupima kiwango cha ufanisi cha walimu na wanafunzi na pia kupima ubora na udhaifu wa mitalaa.

Tathmini iliyofanyiwa mitalaa rasmi ya vyuo vikuu na shule za upili ilizingatia na kufuata hatua maalumu. Kadhalika, tathmini hii ilitarajiwa kufanyika kabla ya mafunzo kuanza, mafunzo yalipoendelea na baada ya mafunzo kukamilika. Kulibuniwa sera maalumu zilizodhibiti mifumo ya tathmini katika vyuo vikuu na shule za upili. Njia kuu za tathmini zilikuwa ni mijarabu na mitihani.

Hata hivyo kwa mujibu wa walimu na wahadhiri walioshiriki katika utafiti, tathmini iliyofanyiwa mitalaa rasmi katika shule za upili ilikuwa ni ya mara kwa mara. Katika vyuo vikuu, tathmini ilifanyika katika vipindi na nyakati maalumu.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

Walimu walieleza jinsi ambavyo tathmini ilichukua nafasi muhimu katika mitalaa rasmi na iliweza kudhibiti shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji.

Ufundishaji wa walimu na wahadhiri na pia ujifunzaji wa wanafunzi ulihusiana moja kwa moja na tathmini kwa kuwa ufanisi wa walimu pamoja na wanafunzi uliamuliwa kupitia kwa matokeo ya mitihani.

Utafiti uligundua kuwa tathmini katika vyuo vikuu ilidhibitiwa na wahadhiri walioandaa silabasi na kuitekeleza darasani. Katika hali hii, wahadhiri walitathmini mada walizokuwa wamefundisha na pia wangeamua kukamilisha mafunzo ya muhula katika silabasi au kutoyakamilisha kwa kuwa wao wenyewe ndio waliandaa mitihani ya mwisho wa muhula.

Katika shule za upili, utafiti uligundua kuwa walimu waliandaa mijarabu na mitihani shuleni ambayo ilitumiwa kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya mtihani wa kitaifa uliofanyika baada ya mafunzo ya miaka minne kukamilika. Mitihani na mijarabu ilipewa kipaumbele katika shule za upili ambapo wanafunzi waliopata alama za juu walipewa zawadi na waliokosa kufikia viwango vilivyohitajika, walidunishwa na kukashifiwa hadharani. Walimu ambao waliwezesha wanafunzi kupata alama za juu walisifiwa kuwa walimu bora na waliopata matokeo duni kutoka kwa wanafunzi wao walikashifiwa kuwa walimu wasiofaa. Hali hii iliwaweka walimu katika mashindano wakijitahidi kuwapa wanafunzi mafunzo bora kufikia kiwango cha kutumia muda wa ziada. Hali kama hii haikutokea vyuoni hivyo basi kuwapa wahadhiri uhuru wa kuutekeleza mtalaa jinsi walivyopenda.

Hali ya wahadhiri kudhibiti shughuli nzima ya tathmini vyuoni ilikuwa na changamoto zake pia kwa vile baadhi ya wahadhiri walitumia mitihani na mijarabu hiyo kwa sababu za kibinafsi; baadhi yao waliitumia kudhulumu au kupendelea wanafunzi ambapo wakati mwingine haikutoa taswira kamili ya uwezo wa wanafunzi. Vilevile kulikuwa na baadhi ya wahadhiri ambao hawakuongozwa na maadili ya kitaaluma katika ufundishaji ambapo walifunza tu baadhi ya mada ambazo walikusudia kutahini. Wahadhiri kama hawa waliishia kufunza kwa lengo la mitihani na wala siyo kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa ambayo yangewasaidia kumudu taaluma zao baadaye. Kwa sababu ya hali kama hizi kutokea miongoni mwa wanafunzi walipopata mafunzo katika baadhi ya kozi, kuna uwezekano kuwa baadhi yao wangekosa kumudu ufundishaji wa kozi hizo. Hivi ndivyo utendakazi wa walimu wa shule za upili uliathiriwa na mfumo wa tathmini uliotumiwa kwao walipoandaliwa vyuoni.

Tathmini ya mitalaa rasmi katika vyuo vikuu na shule za upili iliendeshwa kwa malengo sawa japo tathmini katika shule za upili ilimdhibiti mwalimu lakini katika vyuo vikuu wahadhiri waliidhibiti shughuli. Tathmini ilivyoendeshwa katika vyuo vikuu iliweza kuathiri utendakazi wa walimu walipoutekeleza mtalaa katika shule za upili. Hali hii ilitokea pale ambapo wahadhiri waliandaa mitihani kulingana na mada walizokuwa wamefunza. Ikiwa kulitokea kuwa na mada ambazo hawakufunza na hawakutahini, wanafunzi hawakuzisoma na iwapo zilikuwa katika mtalaa wa shule za upili, utekelezaji wake ungekuwa changamano kwao. Hali hii ingerekebishwa iwapo wahadhiri kutoka vyuo vikuu tofauti wangeshirikiana kuandaa mitihani ifanyike katika vyuo ambako wenyewe hawafunzi.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti uligundua mambo yafuatayo;

Malengo ya utekelezaji mitalaa katika vyuo vikuu ni ya kijumla na hayakulenga maandalizi ya walimu moja kwa moja. Isitoshe, yalitofautiana kutoka chuo kikuu kimoja hadi kingine. Hali hii iliathiri utendakazi wa walimu katika shule za upili ambako walitarajiwa kutekeleza malengo sawa ya mtalaa yaliyobuniwa na TUMIKE.

Vilevile iligunduliwa kuwa walimu hawakujifunza mada zote zilizoorodheshwa katika mitalaa rasmi ya vyuo vikuu ilhali walipofundisha katika shule za upili walitarajiwa kufundisha mada zote zilizokuwa kwenye mtalaa wa TUMIKE. Hili pia liliathiri utendakazi wao kwa kuwa walitarajiwa kufunza baadhi ya mada ambazo hawakujifunza vyuoni.

Utafiti pia uligundua kuwa utekelezaji wa mitalaa vyuoni ulikuwa sawa na ule wa shuleni kwa kuwa wahadhiri na walimu walielekezwa na mikabala, mikakati, mbinu na njia sawa. Utekelezaji wa mitalaa vyuoni ulidhibitiwa na wahadhiri wenyewe ilhali ule wa shuleni ulidhibitiwa na washikadau

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

wengi. Utekelezaji wa mitalaa katika vyuo vikuu uliathiri utendakazi wa walimu shuleni kwa kuwa baadhi yao walifundisha namna walivyofundishwa vyuoni kwa kutumia nadharia, njia na mbinu bila kuzingatia kiwango cha wanafunzi wa shule.

Hatimaye, utafiti uligundua kuwa tathmini vyuoni ilithibitiwa na wahadhiri ilhali shuleni walimu hawakuwa na usemi mkubwa hasa katika tathmini iliyotumiwa kuamua hatima ya wanafunzi. Hali hii iliathiri utendakazi wa walimu kwa kiwango fulani kwa kuwa wao pia waliandaa wanafunzi kwa kulenga sana sehemu walizotaraji kwamba zingetahiniwa.

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulipendekeza kuwa pafanyike mabadiliko ya mara kwa mara ya mitalaa hasa katika shule za upili kwa kuwahusisha walimu pamoja na waandalizi wa walimu ili wakadirie malengo, mada, mbinu za utekelezaji na tathmini mintarafu maandalizi yanayotolewa kwa walimu. Hali hii itawezesha walimu kutoa mchango wao kuhusu changamoto za mtalaa wanaotekeleza na mabadiliko wanayotarajia yafanyike. Kuhusika kwa waandalizi wa walimu kutawawezesha kutoa mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko hayo. Kwa kufanya hivi watawaandaa walimu kuukabili mtalaa vilivyo.

**MAREJELEO**


Adegoke, K. A. (2010). *Why Teacher Education Model Holds the Most Promise for the Nigerian Educational System?* Convocation Lectures for St. Augustines College of Education Akoka, Lagos, Nigeria, pp. 1-23.

Asiimwe, C. (2019). *Mikabala ya Kufundisha.* Katika: Simala, K. I (Mh.). Mitaala ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. Zanzibar: Kakama.

Bilbao, P. P., Lucido, P. I., Iringan, T. C., and R. B. Javier (2008). *Curriculum Development*. Quezon city: Lorimar Publishing, IncBobbit F. (1918). The Curriculum. Boston: Houghton Mifflin.

Brown, J. D. (1995). The Elements of Language Curriculum. A Systematic Approach to Program Development. Boston, MA: Heinle publishers.

Eisner, E (2002). The Educational Imagination: On The Design and Evaluation of School Programs. Upper Saddle River, N. J.: Prentice Hall.

Eshiwani, G.( 1993) *Education in Kenya Since Independence*. East African Educational Publishers, Nairobi.

Flowerdiew, J and Peacock, M. (Eds.). (2001). *Research Perspectives on English for Academic Purposes.* Cambridge. Cambridge University Press.

Goodlad, J. I. (1995). *Ralph Tyler: The Educators' Educator*. Educational Policy, 29(1), 75-81

Goodlad, J. I. (1984). A Place Called School: Prospects for the Future. New York: McGraw Hill.

Hedge, T. (2002). *Teaching and Learning in the Language Classroom* (3rd Ed). Oxford: Oxford University Press.

Kafu, P. A. (2013). *Teacher Education: the Incubator of Science and Technology for Development in Africa.* African Journal of Education Science of Technology (AJEST), 1(1), 1-14.

King'ei, K. (2001). *From the Real to the Ideal: Survey of Kiswahili Curricular in East Africa's Universities.* Kiswahili in the 21st Century,179 2000 Publisher for Advanced Studies of African Society.

Lynch, D. E. (2003). So You Want to Make a Real Difference: An Introduction to Learning Management for the Teacher in Training. Monograph: Central Queensland

Makoti, V. (20017). Ufundishaji wa Kiswahili na Changamoto zake Mintaarafu Chuo Kikuu cha Moi. Katika Jarida la Mwanga wa Lugha. Juzuu Na. 1, uk. 111 – 122.

Mbuthia, F. K. (1996). Comparative Study of the Effects of Two Instructional Approaches on Students' Performance in Kiswahili Poetry in


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

Selected Secondary Schools in Eldoret Municipality. Unpublished Master's Thesis, Moi University.

McArthur, L. Z. and Baron, R. M. (1983). *Toward an Ecological Theory of Social Perception*. Psychological Review, 90(3), 215–238.

Miller, L and Silvernail, D. (2000). *Learning to Become a Teacher: the Wheelock way*. In L. Darling Hammond (Ed), Studies of Excellence in Teacher Education. Preparation in the Undergraduate Years. Washing D.C: American Association of college for teacher education.

Musau P. (2002). *Polemics Versus Reality: Bridging the Gap in Kiswahili Research*. In: K.Inyani Simala(Mh.) Utafiti wa Kiswahili.CH AKITA. Eldoret, Moi University Press.

Musungu, L. L. and Nasongo, J. W. (2008). The Head-teacher's Instructional Role in Academic Performance in Secondary Schools in Vihiga District, Kenya. Educational Research and Review, 3(10), 316-323.

Mutiga, J. (2008). *Nature and Nurture: Tenets in the Acquisition of Kiswahili as a Second Language in the Kenyan Bilingual System of Education*. In: Ogechi,N. et.al (eds).Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika (pp.397-405) ISBN 9966-854-47-9, Moi University.

Nasimiyu, G, (2017). *Preparation of Teacher Trainees in Pedagogy in Kenyan Universities*. Journal of Education and Practice,V8 n 13 pg 28-34.

Oliver, A. I. (1982). Curriculum improvement. A guide to problems, principles and processes. (2nd ed.) New York: Harper & Row Publishers.

Oluoch G. P. (2006). *Essentials of Curriculum Development*. Nairobi Longhorn Publishers.

Otunga, R. N. (2010). The Dilemma of Curriculum Relevance in Kenya. Eldoret: Moi University Press.

Oyedeji, N. B. (1998). *Management in Education, Principles and Practice*. Lagos: Aras Publishers.

Shiundu, J. S. and Omulando, S. J. (1992). *Curriculum: Theory and Practice* in *Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Simala K. I. (2019). *Uhuishaji wa Mitaala ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki*. Katika: Simala, K. I. (Mh.). Mitaala ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Zanzibar: Kakama.

Simala, K. I. (2013). *Critical Pedagogy and Kiswahili Education. Challanges and way Forward*. In: Egara K. na wengine. New Horizons in Pedagogy. Kakamega. MMUST University, Kenya.

Simala, K. I. (2002). *Miradi ya Utafiti katika Vyuo Vikuu Mnamo Karne ya Ishirini na Moja*. Katika: Simala K. I. (Mh) Utafiti wa Kiswahili. Eldoret: Moi University Press

Sitima, T. M. (1995). *Maintainance of Standards in Teacher Education*. In: Ministry of Education. Report of Proceedings of the 3rd Teacher Education Conference. Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Taba, H, (1962). *Curriculum Development.* New York: Hacourt, Brace and World.

Taba, H. (1962). *Curriculum Development Theory & Practice*. New York. Harcourt: Brace & World.

Tyler, R. W. (1949). *Basic Principles of Curriculum and Instruction*. Chicago: University of Chicago Press.

University of Nairobi. (1978). *A Review of Graduate Teacher Evaluation in Kenya*. Nairobi: University of Nairobi.

UNESCO (2011). *The Hidden Crisis: Armed Conflict and Education*. Background paper prepared for Education for All Global Monitoring Report.Paris, UNESCO.

Urevbu, A. O. (1994). *Curriculum Studies* (2nd ed.). Singapore: Longman.

Urevbu, A. O. (1985). *Curriculum Studies*. Ikeja: Longman.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.556

Wagari, S. (2003). Problems Facing Teacher Education in Kenya: A Case Study of Teaching Practice in the University of Nairobi. Unpublished Master's Thesis, University of Nairobi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.